

# 3 Yohana



# Contents

Salamu1 Gayo Anasifiwa Kwa Ajili Ya Ukarimu Wake1 Deotrefe1 Demetrio1 Salamu  
Za Mwisho1



# 3 Yohana

Salamu

1Mzee:

**K** wa Gayo rafiki yangu,  
nimpendaye katika kweli.  
Gayo Anasifiwa Kwa Ajili Ya  
Ukarimu Wake

2Mpendwa, naomba ufanikiwe  
katika mambo yote na kuwa na afya  
njema kama vile roho yako  
ifanikiwavyo. <sup>3</sup> Ilinifurahisha sana  
baadhi ya ndugu walipokuja na  
kutueleza juu ya uaminifu wako  
katika kweli na jinsi unavyoendelea  
kuenenda katika hiyo kweli. <sup>4</sup> Sina  
furaha kubwa kuliko hii, kusikia  
kwamba watoto wangu wanaenenda  
katika kweli.

5Rafiki mpendwa, wewe ni  
mwaminifu kwa yale unayowatendea  
ndugu, ingawa wao ni wageni kwako.

<sup>6</sup> Wameshuhudia kuhusu upendo  
wako mbele ya kanisa. Utafanya  
vyema ukiwasafirisha kama  
inavyostahili kwa Mungu. <sup>7</sup> Ilikuwa  
ni kwa ajili ya hilo Jina waliondoka,  
bila kukubali kupokea msaada  
wowote kutoka kwa watu  
wasioamini. <sup>8</sup> Kwa hiyo imetupasa  
sisi kuonyesha ukarimu kwa watu  
kama hao ili tuweze kutenda kazi  
pamoja kwa ajili ya kweli.

Deotrefe

9Niliandikia kanisa, lakini  
Deotrefe, yeye apendaye kujifanya  
wa kwanza, hakubali mamlaka yetu.  
<sup>10</sup> Hivyo kama nikija, nitakumbuka  
matendo yake atendayo, akitusingizia  
kwa maneno ya hila. Wala hatosheki  
na hayo anayotusingizia, bali pia  
hukataa kuwakaribisha ndugu, na  
hata huwazuia wale walio tayari  
kufanya hivyo na kuwafukuza  
watoke kanisani.

Demetrio

11Rafiki mpendwa, usiige lile lililo  
baya bali lile lililo jema. Yeyote  
atendaye mema atoka kwa Mungu,  
bali atendaye mabaya hajamwona  
Mungu.

12Kila mtu ameshuhudia mema  
kuhusu Demetrio, vivyo hivyo hata  
na hiyo kweli yenyewe. Sisi pia  
twashuhudia mema juu yake, nanyi  
mwajua kwamba ushuhuda wetu ni  
kweli.

Salamu Za Mwisho

13Ninayo mambo mengi ya  
kukuandikia, lakini sipendi kuandika  
kwa kalamu na wino. <sup>14</sup> Badala  
yake, nataraji kukuona upesi, nasi  
tutaongea pamoja ana kwa ana.

15Amani iwe kwako. Rafiki zetu  
walioko hapa wanakusalimu.  
Wasalimu hao rafiki zetu walioko  
huko, kila mmoja kwa jina lake.